

* CHECK FOR KILUGA, TRANSCRIPT COMPLETE FOR SWAHILI, Tape #160

160 COMPLETE

{TAPE # 160, DONE BY NYAMUSI MAGATTI, AUGUST, 2009}

{SIDE A}

Mwita: {kilugha}

A: hiyo ilikuwa ni summary tu, jina anaitwa Mwita

Nyamgamba: anaitwa Mwita

A: Maro

Nyamgamba: Mosi, Mosi nani?

Mwita: Mosi Sasi

Nyamgamba: Sasi nani?

Mwita: Sasi Wesinge

Nyamgamba: Wesinge haha Wesinge?

Mwita: Wesinge Machage

Nyamgamba: Machage?

Mwita: Machage Nyarutare

Nyamgamba: Nyarutare?

Mwita: Sarigoko

Nyamgamba: Sarigoko

Mwita: Sarigoko Rutorora

Nyamgamba: Rutorora

Mwita: Rutorora Mumbia

Nyamgamba: Mumbia haha

Mwita: Mumbia Mmare

Nyamgamba: haha sawa aah kumbe hatujampata huyu mtu Mmare sawa hamati yako?

Mwita: hamati yangu ni Mmare, ndio tumetoka kwa Mmare huyu

Nyamgamba: haha nimesikia kuna wamare ambao ni wasweta wamare waeregi wamare wa aina nyingi?

Mwita: Mmare, lakini ni mwiregi Mumbia

Nyamgamba: Mumbia ni huyu motto wa Mmare

Mwita: eeh (laughing)

Nyamgamba: haha sawasawa zinaingiliana

Mwita: zinalingiana

Nyamgamba: sawa rikora yako?

Mwita: Maina..

Nyamgamba: aah wewe ni upande wa chuma?

Mwita: hapana wasai

Nyamgamba: wasai aah hawa ni watoto wa hawa wagamunyeri haha

Mwita: wamasaai

Nyamgamba: haha na sega yako ?

Mwita: Maina
Nyamgamba: aah samahani saro yako?
Mwita: umuruka
Nyamgamba: umuruka haha
Mwita: saro ya kina baba
Nyamgamba: hii ni yako?
Mwita: eeh ndio hiyo ni yangu
Nyamgamba: na ilikuwa mwaka gani mlifanya?
Mwita: arubaini na mbili ndio saro yangu
Nyamgamba: haha ni hii saro yako ni katika upande gani wa sega wa burumaranja, bungererati?
Mwita: busahi
Nyamgamba: busahi haha sawa
Mwita: {kilugha} omusai
Nyamgamba: omusai sawa.. unaweza kujua mwaka wa kuzaliwa?
Mwita: 1924
Nyamgamba: ulizaliwa wapi?
Mwita: hapa hapa Bumare
Nyamgamba: Bumare sehemu gani?
Mwita: Bitakonga
Nyamgamba: Bitakonga haha halafu ukahama sehemu nyingine au ni?
Mwita: sijabadilisha kwenda mahali pengine ni hapahapa
Nyamgamba: au ulienda nje kwa kazi au?
Mwita: kwa kazi nilikwenda nje?
Nyamgamba: ulienda wapi?
Mwita: Geita
Nyamgamba: haha ukafanya kazi gani?
Mwita: aah nilikuwa nachukua mchanga ndani ya mine
Nyamgamba: haha ilikuwa mwaka gani?
Mwita: 1939
Nyamgamba: haha mpaka mwaka gani?
Mwita: mpaka arubani na sita nikatoka
Nyamgamba: mmh ulikaa sana?
Mwita: ndio
Nyamgamba: ulienda sememu nyingine?
Mwita: Mwadui
Nyamgamba: mpaka
Mwita: hamsini noti
Nyamgamba: haha ulikuwa na kazi ileile
Mwita: hapana hapo nilijifunza udereva, mwaka arubaini na nane
Nyamgamba: kwahiyo ulipoenda Mwadui ulikuwa dereva?
Mwita: aah nimeanzia huko
Nyamgamba: haha halafu ukafanya nini?
Mwita: nikarudi hapa nyumbani

Nyamgamba: mwaka?

Mwita: mwaka nilisema hamsini

Nyamgamba: aah ndio ulirudi kwasababu baba alikuomba urudi au uliona tu?

Mwita: niliona nije nikapumzike nikaoe

Nyamgamba: haha ulikuwa bado kuoa

Mwita: nilikuwa bado kuoa

Nyamgamba: haha baba alikuwa bado yupo?

Mwita: eeh baba alikuwa yupo

Nyamgamba: na mama wote?

Mwita: wote

Nyamgamba: sawa kwahiyo baada ya kurudi nyumbani ulishika kazi nyingine hapa?

Mwita: niliendelea kukaa nyumbani hapa, kuwa mtemi Simeo

Nyamgamba: messenger? Mwaka hamsini na?

Mwita: na mbili

Nyamgamba: na mbili

Mwita: mpaka hamsini na tatu, hamsini na nne nikarudi tena Musoma

Nyamgamba: haha

Mwita: {kilugha}

Nyamgamba: aah sawa halafu

Mwita: sasa nikakaa pale Musoma kwenye mwaka hamsini na nne mpaka mwaka sitini ndio nimeacha kazi pale Musoma nikaja nyumbani hapa

Nyamgamba: ukaona hapa nyumbani?

Mwita: eeh nikaoa, sasa mzee akafariki

Nyamgamba: haha sawa na uliporudi nyumbani ukashika cheo Fulani?

Mwita: nikaendelea kuwa mwenyekiti wa muda kama miaka mitatu

Nyamgamba: mwenyekiti wa?

Mwita: wa kijiji

Nyamgamba: kijiji...mpaka mwaka gani?

Mwita: sabini na tatu#sabini na sita

Nyamgamba: na baada ya kuacha uenyekiti?

Mwita: nikakaa hapa nyumbani, mahakama nimefanya kama miaka mitatu

Nyamgamba: haha sawa na upande wa mila na desturi ulikuwa na unafanya ulipata cheo chochote labda kwenye nyangi au mambo mengine

Mwita: sijapata cheo

A: amekabidhiwa#

Mwita: hiyo nayo ni cheo..kupiga baragumu

Nyamgamba: haha kupiga baragumu

A: amekabidhiwa baragumu ya rikora

Mwita: {kilugha}

Nyamgamba: hiyo ndiyo baragumu ya rikora?

Mwita: eeh

Nyamgamba: eeh kumbe inatengenezwa hii ni ya ng#ombe au ni nini?

Mwita: ni mnyama gani?

A: Mngirisi {kilughaa}angalia

Nyamgamba: aah nitapiga picha kabisa

Mwita: haha hii ndio tandara mpaka hapa, ndio ile mpaka pale ndani lakini hii ni nyati..

Nyamgamba: nyati haha#kwahiyo ulisema inapigwa wakati gani?

Mwita: wakati kama ng#ombe zimeibiwa, wakati wa vita au wakati wa hatari

Nyamgamba: ukitaka kuita mkutano unaweza?

Mwita: ndio, inapigwa saa kumi na mbili ya jioni na saa kumi na mbili asubuhi

Nyamgamba: haha na bado unaitumia au hapana

Mwita: si ndio naitumia

Nyamgamba: lakini unaipiga

Mwita: nalipuliza

Nyamgamba: kama ngome zinaibiwa hata leo ungeipiga?

Mwita: naipiga hata sasa wakisema kama nimesikia

A: kama ile tarumbeta

Mwita: tarumbeta kama ya jeshi

Nyamgamba: sasa ulikabidhiwa mwaka gani?

Mwita: hii nimekabidhiwa mwaka# hamsini na saba

Nyamgamba: hamsini na saba..na asaro yako ilikuwa mwaka?

Mwita: arubaini na mbili

Nyamgamba: arubaini na mbili, hiyo haikuwa kwenye saroyako?

Mwita: sikukabidhiwa kwenye saroyangu, ilikuwa bado

Nyamgamba: kwahiyo ilikuwa kwenye saroyakina nani ulikabidhiwa?

Mwita: wa baba zangu

Nyamgamba: lakini ni?

A:{kilugha}

Mwita: ilikuwa sio nyangi, siku hiyo ilikuwa ni mkutano wao wanakwenda kumsaidia

Manangokowalisema leo tumechoka leo vijana wetu, tulikuwa wasare wote

Nyamgamba: haha

Mwita: kwahiyo ilikuwa ni kama sherehe, yeyé alipewa na wamare tu

Nyamgamba: na wamare, wagamunyeri na wamare

Mwita: eeh maana hii ni yakwetu tu wamare na kila kabila, kila koo hapa ina yao

Nyamgamba: mmh haitegemi kwamba ni wamare wa abairegi au wamare wa nini na nini, ni wamare wote?

Mwita: haha hii ilikuwa ni wamare, tuseme zilikuwa ni kabila hii mbili na ile ya mnyama ilikuwa ya tatu kwahiyo sasa hii moja ilikuwa kwa huyu na nyingine tena ndogo yake ilikuwa kwa Werege

Nyamgamba: hakuna nyingine?

Mwita: ziko tatu

Nyamgamba: kwa wamare?

Mwita: eeh kila kabila kwetu hapa au kila mlango unataka uwe nazi hivi..vitatu

A: huwa ziko nne, huwa na ile tarumbeta, kadogo kale vijana wadogo wadogo wanapewa

Mwita: tarumbeta

Nyamgamba: mmh kwahiyo wanazigawanaje?

Mwita: kwenye nyumba Weregi

Nyamgamba: Weregi wanayo moja

Mwita: moja, Weregi ya ukoo wa huyu walikuwa nayo moja na sisi Weregi tulikuwa nazo mbili

Nyamgamba: kuna Waeregi wa aina mbili?

Mwita: Weregi wa aina mbili

Nyamgamba: kwahiyo Waeregi wa kwenu wanaitwa Waeregi nani?

Mwita: Waeregi wa abahiri Mumbia

Nyamgamba: abahiri Mumbia haha na waeregi hawa wengine wanaitwa?

Mwita: {kilugha}

Nyamgamba: barimande haha kwahiyo watatu kwa..

Mwita: wa kiseru wapo {kilugha}

Nyamgamba: kwahiyo abakiseru wana moja?

Mwita: eeh

Nyamgamba: ya wamare haha na ya wane?

Mwita: wanne wasweta

Nyamgamba: wasweta haha lakini hii ilikabidhiwa tofauti na hizi zingine?

Mwita: wao vilevile wanakabidhi kulingana na siku ile inakabidhiwa ni wote tulipewa, sasa wakatoka akina baba wakatuachia sasa {kilugha}

Nyamgamba: haha

Mwita: {kilugha}

Nyamgamba: na ulikabidhiwa mambo mengine siku ile?

Mwita: aah hapana

Nyamgamba: ile nyama?

Mwita: nyama hii ya kuchukua juzi, tulikuwa tunakula wakati tunakabidhiwa

A: huku kwenye makabidhiano sasa vijana wanakula nundu

Nyamgamba: sawa

Mwita: wanakula nundu ya ng#ombe

Nyamgamba: mmh

Mwita: na wazee wanakula mgongo, sasa tuendeleo hapo nyama za mgongo halafu wazee wakubwa wazee wakora nyangi wanakula sarara

Nyamgamba: sarara ni wapi?

Mwita: sarara ndio nyama hizi laini, hizi za humu

Nyamgamba: aah na kichwa nani anakula?

Mwita: aah hiyo thamani

Nyamgamba: haina haha

Mwita: sarara nyama laini sawa sasa hapa uje uandike vizuri hawa ni wakora nyangi halafu hawa ni wazee wa makamu

Nyamgamba: sawa

Mwita: eeh sasa hawa ni vijana, sasa yeye wakati amepewa hii alikuwa yuko hapa bado hapa kwasababu huyu nimekuambia ndio mtangi wa wagamnyeri

Nyamgamba: mmh na mtangi wa?

Mwita: wagamnyeri

Nyamgamba: wa Maina?

Mwita: wa wagamnyeri

Nyamgamba: aah mtangi wa

Mwita: mtangi si ni motto wa kwanza, ndio Maina sasa huyu ndio mkubwa wetu wote

Nyamgamba: haha sawa kwahiyo kazi yako kama wewe ni mtangi ni nini?

Mwita: sasa mimi ni mtangi kwakuwa mimi ni mtu mkubwa kwa sasa hivi mwaka juzi ndio tumekabidhiwa sasa mgongo tunaanza sasa kwenda polepole tunakuja kung#atuka sasa ila hii bado hatujakabidhi vijana wetu ila sasa tumeshakula mgongo tumehama kwa hiyo

A: kung#atuka kutoka kwenye nundu tunakuja kwenye mgongo, uking#atuka kwenye mgongo unakuja kwenye sarara

Nyamgamba: kwahiyo wakati wazee wanang#atuka wao wanaenda kula mgongo wanaachia nyinyi

Mwita: eeh wanawaachia vijana sukubi

Nyamgamba: haha

A: hapo labda tueleze kuwa unapokuwa kijana unakula sukubi

Mwita: basi angalia mfano mzuri hapa unapokuwa mzee wa makamu unakula mgongo, unapotoka kwenye uzee sasa unaenda kwenye uzee kabisa unakula sarara

Nyamgamba: sawa

Mwita: na wanalia watu, huwa kuna sehemu ya kulia, si ovyo ovyo

A: kuna vyombo vyake

Nyamgamba: haha sawa

Mwita: sukubi inaliwa ndani ya zizi {kilugha} nje ya zizi kwenye ekehita, halafu mgongo inaliwa ndani katikati ya zizi, sarara inaliwa kwenye ghala

Nyamgamba: kwenye ghala

Mwita: kama pale wanakaa pale halafu sinia yao ni orohongo

Nyamgamba: haha

Mwita: lakini hapo palikuwa pazuri

Nyamgamba: haha sawa kwahiyo ulikuwa unasema wewe kama mtangi wa wagamnyeri shughuli yako ni nini? Akipiga yeyé ni kosa?

Mwita: anaweza yeye baragumu kwa haraka kama kuna hatari, wanauliza kulikuwa na hatari gani?

Nyamgamba: lakini mtu mwingine hawezi kupiga au ni wewe tu?

Mwita: kama siku tuna kikao au mkutano mkuu anajifunza tu

Nyamgamba: haha sio mbaya

Mwita: sio mbaya, lakini huwezi ukaipiga hivihivi mpaka siku ya matukio

Nyamgamba: mmh kitu ambacho nilitaka kujua ni kama huyu mtangi ana wajibu wowote katika ulinzi wan chi kwa jumla au?

Mwita: kwa ukoo wao ni mtu kama anaheshimiwa au kama kuna shughuli Fulani unaweza kusema wewe pamoja na huyu nani mkubwa Fulani nenda wewe utuitie mtu Fulani pale eeh sasa akikataa wanasema yani unatumwa na mtu mkubwa unakataa eeh

Nyamgamba: na wakati wazee waling#atuka walikufundisha mambo mengine ambayo ni wewe ambao unakabidhiwa una..?

Mwita: ipo nyangi ambayo tunaifanya kama hawa hawajaifanya yani kuporona, ndio nilishakuonyesha namna ya mila kuporona

Nyamgamba: ulifanya eborana?

Mwita: eeh nilifanya eborana

Nyamgamba: na walikufundisha mambo ambayo bado unaitumia?

Mwita: nayatumia kwa mazingara waliyonifundisha

Nyamgamba: haha..na inahusu kazi yako ya mtangi au hapana?

Mwita: hiyo inahusu mila na desturi kwa wangoremi waliotairi borana kama siku ikitokea mahali fulani wewe umefika ndio unaonyesha

Nyamgamba: na kama wewe umeborana unaweza ukaborana motto wako au?

Mwita: ndio

Nyamgamba: unaweza ukafanya?

Mwita: ninaweza nikafanya kwa mzee yeyote atakayefanya ananizidi analeta watoto , nachukua kama huyu wa kwangu nampereka anakwenda kuborana kabla mimi sijaifanya hapa

Nyamgamba: mmh aah sawa na kuna mengine ambayo walikukabidhi siku ile?

Mwita: hapana

Nyamgamba: ni hii, na ulisema siku nyingine ulipata nyama kukabidhiwa?

Mwita: eeh

Nyamgamba: si siku ile?

Mwita: si siku ile

Nyamgamba: haha na wanachagua siku yoyote ambao wamekusanyika?

Mwita: ni siku wanaokusanyika wanaona hiyo kitu, hao wanafuatwa

Nyamgamba: hawakuita sherehe?

Mwita: hawakuita

Nyamgamba: maalum?

Mwita: eeh hawana sherehe maalum, kama hiyo waliona

Nyamgamba: na hii inaitwa kuteneka au hapana?

Mwita: hapana

Nyamgamba: ni tendo gani?

Mwita: ni kitu wanaona tumefika umri tumekuwa idadi Fulani tumekomaa, hata mimi leo naweza kusema tuchukue vijana wa huyu na huyu jamani ng#oma yenu ni hii tunang#atuka kama sasa tumefika ila ni watoto wanaogopa ogopa kila siku tunawaambia jamani ng#oma yenu ni hii lakini wanaogopa

Nyamgamba: aah wanaogopa?

Mwita: aah mimi sijui, mwingine anasema haha tunasema basi

Nyamgamba: na mtangi wao mmeshajua ni nani?

Mwita: mtangi tunaujua tu, yupo mkubwa

Nyamgamba: haha na yeye anakataa?

Mwita: anaogopa (laughing) sasa anarudi tena kusema wapo wa kwangu anamzidi huyu kidogo anajua kutandika, jamaa huyu aendeleo kukaa nayo maana yeye ameshaifahamu

Nyamgamba: eti ina hatari yake kwanini anaogopa?

Mwita: anaogopa shauri ya kulitimisha

Nyamgamba: aah ni ngumu?

Mwita: ni ngumu aah

A: hiyo ni sawasawa na kamanda wa jeshi, yeye anakuwa na sauti kubwa

Nyamgamba: hii ambayo nilitaka kujua kwahiyo anaogopa kuna dawa au kuna nini?

Mwita: maana humu ikipigwa tumbo yako inafanya nini {kilugha}, kuna ngozi ya simba humu ya ng#ombe, katikati kuna ya simba

Nyamgamba: na kuna madawa madawa ndani yake

Mwita: eeh ndio nakwambia..

Nyamgamba: na ni juu yako kuifanya iwe upya tena au unaiacha iwe hivyo?

Mwita: haha mimi ni kupenda kutaka kuwa upya labda ikitokea mila na desturi ya huyu amefanya tuseme sherehe ninaweza nikaenda nikawaambia wanatoa mkono wa kulia halafu naleta nachunika humu inatolewa hivi halafu inawekwa humu, kama hapa unaona wadudu wamekula

Nyamgamba: kwahiyo ulipokabidhiwa ukapata siri za dawa yake?

Mwita: eeh waliniambia

Nyamgamba: kwahiyo ukikabidhi kwa mwingine na yeyé anapata siri hizo?

Mwita: eeh namwambia siri hizo eeh

Nyamgamba: na kuna mitambiko fulani unahitaji ufanye wakati huo

Mwita: aah haitaji siku hiyo wakikukaliza wamekukaliza hamna mitambiko yoyote

Nyamgamba: haha na huna mitambiko ambayo lazima ufanye unapoitunza?

Mwita: hata

Nyamgamba: haha

Mwita: hapa ni kukabidhiwa unakwenda nayo, hata mimi nikimkabidhi kijana hao wote tumekubali leo kijana fulani ngoma yenu ni hii umeng#atuka basi wanakwenda nayo

Nyamgamba: na kwa bahati mbaya ikiharibika kuna madhara yoyote inatokea?

Mwita: ni kuripotiana siku hiyo hii tunasema ni tandara

A: {kilugha}

Mwita: ile tandara inatolewa ile ya kulia basi inachongwa sihitaji tena utafute hii kama hii ilikuwa ni ngumu unatafuta nyingine safi tena unakuja unaunga tofauti na hii

Nyamgamba: lakini ni wewe unahitaji kutengeneza?

Mwita: mimi mwenyewe

Nyamgamba: haha labda hii ni maana kijana anaogopa?

Mwita: (laughing)

Nyamgamba: aah kumbe sawa

Jan: basi tuendeleo na historia ya Wamare

Nyamgamba: sawa

Mwita: kwenye mto Bumeti akabaki Mwikoma kule ng#ambo walikuwa vijana wawili, mngoremi akaja huku ng#ambo yani huku kwetu pamoja na manjia sasa akateremka nayo

Nyamgamba: nani?

Mwita: Mungeremi

Nyamgamba: mungeremi ni nani?

Mwita: Mkoma alibaki huko Ikoma kule na Mungoremi akaja huku

Nyamgamba: sawa samahani sasa endelea kuhusu Ngurime akafanya nini?

Mwita: mngoremi sasa akazaa hapo akapata nyingi nyingi hizo wamare, kitale ikawa Ngoremi nzima sasa ikapatikana humu milango milango mwiregi eeh wakateremka kuja kwenye milima milima zaidi ya hapo sasa sijaendelea kufahamu vizuri

Nyamgamba: hujui labda majina ya wengine ambao walikuwa wametoka huko wakaja

Mwita: mmh mimi najua walipotoka sasa kuwatanyika tena wengine wakatoka sehemu hizi sasa hapo siwezi kufahamu

Nyamgamba: mmh hawa ambao wanataja huyu Sabayaya ni nani?

Mwita: Sabayaya ndio sisi hawahawa tuliotoka, tulipotoka huku Mangweso tukaja sehemu ya Sabayaya wangoremi wa Sabayaya

Nyamgamba: haha hii Sabayaya ilikuwa baada ya mngorime au kabla ya Ngorime?

Mwita: Sabayaya alikuwa ameshatoka sasa

A: {kilugha} kwa maana hiyo la kwanza ilikuwepo

Mwita: {kilugha}

A: nafikiri huyu Sabayaya ndio amemzaa Wandira

Nyamgamba: haha

Mwita: sio ndi ni Warira

Nyamgamba: Warira haha

A: tukirudi hapa tunaweza tukapata..

Mwita: {kilugha}

A: nilichokuwa nakitafuta kimepotea maana nilitaka kujua kwamba wangoremi wametoka wapi nimeshapata kwa msingi huo huyu Sabayaya ni kijana, Wandira, Sabayaya Wandira kwa maana huyu ni baba, huyu ni mtoto wake

Nyamgamba: sawa lakini hatujui kwamba..

{END OF SIDE A}

{START SIDE B}

A: ile ya kwao nafikiria huyu Sabayaya amezaa Wandira, Wandira huyu maana sisi wangoremi ndio tunajiita hivyo kwa msingi ni kwamba huyu Wandira ndiyo amemzaa Wangoremi, nina wasiwasi kitu kama hicho

Nyamgamba: na kuna mlima hapa ambayo inaitwa Isabayaya ambayo huyu mzee alitaja?

Mwita: si alisema pale au mimi ndio sikuelewa

Nyamgamba: aah ndio alisema kuna mlima

A: hii sabayaya sijaisikia

Mwita: {kilugha} hiyo lakini sijui kama kuna mlima hapa

A: {kilugha}

Nyamgamba: sawa sasa ulisema kwamba mlikuwa pamoja na wa Ikoma sasa hata wa Ikizu wana historia kwamba na huyu mtu wao wa kwanza akaenda huko Mangwesi akampata sijui nani Sabayaya halafu akarudi tena Ikizu sasa na ninyi mna historia hiyo?

Mwita: huyu Sabayaya ndiyo huyu huyu ametokea hukuhuku Sabayaya ndio akaja kuzaa sisi hapa inaitwa Sabayaya

Nyamgamba: haha sawa na kwa wamare ni hawa tu ambao wametoka Sonjo au kuna wengine walikuja kuingia baadaye?

Mwita: walipookuja hapa wamare wakawa wanagawanyika sasa, eeh kukawa na vijana watatu mwingine ana mji wake na kujiita mimi..

A: {kilugha}

Mwita: {kilugha}

Nyamgamba: abasweta na?

Mwita: abasweta na abahiri magita

Nyamgamba: magita? Hawa wametoka wapi?

A: abasweta wametoka nafikiri ni Tarime, ni eneo la Kenya

Mwita: wametokea Kenya {kilugha}

A: halafu hawa nafikiri wametokea Uganda hawa

Mwita: [kilugha]

A: hii imetokea Uganda

Nyamgamba: kwahiyo hawa wote wamare wote ambao asili ya ni kutoka Soncho wanaitwa waeregi?

Mwita: [kilugha]

Nyamgamba: lakini wote ni wamare?

Mwita: wote ni wamare

Nyamgamba: haha na ni wamare kwasababu wanakaa eneo hilo?

Mwita: eneo hilo

Nyamgamba: la Bumare?

Mwita: la Bumare

Nyamgamba: haha

Mwita: ni sehemu imetoka huko juu mpaka Rusinga, wamepakana

Nyamgamba: kwahiyo Bumare inaenda mpaka inafika Nguko?

Mwita: aah hapana, mwisho ni hapa kwenye kamlima hapa, inapakana na wanguko halafu inakwenda huku na huku tunapakana na Kitale

A: ila utakapokwenda sehemu ya White brothers utakuta kuna Bumare 1 na Bumare 2, sasa ile ramani mariwani la Bumare 2 itakuja kukufikisha kwakuwa wewe umetembelea itakuja kukufikisha karibu na Bantamome eneo la mwisho kwasababu walikuwa eneo hilo kama ni ni mrambaro wanne

Nyamgamba: haha

Mwita: maana hiyo milima ya Mrambano 1 hiyo ilikuwa inamilikiwa kihimaya sasa kiutawala ilikuwa chini ya Bumare

Nyamgamba: ya Bumare?

Mwita: ee kiutawala

Nyamgamba: sawa na ukichunguza ndani zaidi ni kama Bumare ni nchi lakini kitu kama waeregi au nini ni ukoo lakini unaweza kusema wamare ni ukoo au si ukoo maana wana ujamaa au ni watu mchanfganyiko tu ambao wanakaa pamoja?

Mwita: Wamare tunasikia ni wakitale lakini wako vinyumba vinyumba vinyumba, milango sasa na sisi Wamare wote ni Wamare

Nyamgamba: haha sawa

Mwita: sasa kwenye kugawanyikana utakuta wamo Waeregi, wasweta hapohapo tena utakuta ni Mwiregi eeh

Nyamgamba: haha kwa mfano wamare wanaenda wapi kusengera?

Mwita: wote tunakwenda huko juu milima yetu

Nyamgamba: haha kwahiyo wote mnaenda kwa pamoja?

Mwita: wote pamoja

Nyamgamba: hata kama ni mlango gani?

Mwita: Bumare hii ya kwetu ni wasai na bungerati ukitaka kwenda kusengera huku tunakwenda siku hii, moja tunapiga baragumu hapa na huku wanapiga tunakuja tunakutana hukuhuku juu

Nyamgamba: na inaitwa wapi wanaenda?

Mwita: Sengere

Nyamgamba: Sengere

A: kuna sehemu mbili, kuna Sengere kuna Nyakigumo
Mwita: Nyeremanda
Nyamgamba: Nyakigumo
A: sasa hapo umeandika
Nyamgamba: Nyakisengere, Nyakigumo
A: halafu kuna Remande
A: mmh sasa weka dash hapo sasa hii Sengere {kilugha}
Mwita: {kilugha} kwanza tunajikusanya tunaenda wapi, tunaenda Sengere tukitoka Sengere
Nyaute, Nyagekenge tukishatoka Nyagekenge
Nyamgamba: haha kwahiyo mnaanza Sengere halafu
Mwita: Sengere
Nyamgamba: halafu mnaenda?
Mwita: Nyeute
Nyamgamba: Nyeute halafu mnaenda?
Mwita: Nyegekenge
Nyamgamba: Nyegekenge halafu?
Mwita: tunagawanyikana sasa Warimande wanakwenda Remande
Nyamgamba: warimande
Mwita: wanakwenda Remande
Nyamgamba: wanaenda Remande haha
Mwita: wakisero wanakwenda Romo pamoja na Wasweta
Nyamgamba: haha sawa
Mwita: Walimagure wanakwenda Kitachi na Nyahute {kilugha}
Nyamgamba: wanaenda Kitachi na?
A: Nyahute
Mwita: {kilugha}
Nyamgamba: Rematomano
Mwita: sawasawa tunagawanyikana sasa
Nyamgamba: mmh
Mwita: {kilugha} tunakuja kukutana tunateremka huku
Nyamgamba: mnakutana wapi tena?
Mwita: tena tunateremka sasa kuja hapa kama kuja Bumare hapa kwenye kijiji
Nyamgamba: na yote inafanyika siku moja?
Mwita: ni siku hiyo hiyo tu
Nyamgamba: aah
A: anyway baada ya kumaliza sehemu kuu hizi Sengere halafu tunatoka wote Sengere
tunakwenda Nyahute tunatoka wote Nyahute tunakuja Nyegekenge sasa tukishafika hapa hii
nyumba kubwa, unajua hapa sasa kuna nyumba mbili, nyumba kubwa ambayo ni abahiri
mombia hawaendi sehemu yoyote ile
Nyamgamba: abahiri mombia ambayo ni nyumba kubwa haha
A: hawa wanakaa sasa hivi nyumba ndogo zinatawanyika sasa kwenda kuiji maana hii ni kuiji
wanakwenda sasa kuiji kwenye vyumba vidogo vidogo yao
Nyamgamba: kuhiji?
A: kuhiji sasa ni kuabudu

Nyamgamba: aah sawasawa na mnafanya nini hii sehemu zote mnafanya mitambiko gani?
Mwita: mitambio hapo utakuta wengine wana tumbaku wana maunga wanatambikia pale kuna maji yanchotwa mle, sasa ndio wanakuja
Nyamgamba: lakini kuchinja mnachinja huko?
Mwita: tunachinja mbuzi hapohapo Sengera
Nyamgamba: Sengera?
Mwita: Nyagikenge
Nyamgamba: haha
Mwita: {kilugha}
Nyamgamba: kwahiyo abahiri mombia wanabaki palepale mahali ambapo mnachinja?
Mwita: eeh tunangoja hawa waende kutambika huku halafu wanakuja sasa tunateremka sasa kuja chini
A: halafu wanakuwaga na mbuzi wawili, wanatoa huku mbuzi moja na kule wanatoa mbuzi moja
Nyamgamba: haha sawa na mnapofanya hii kitendo hii ambacho Wamare mnaenda, mnaenda kuomba nini?
Mwita: kuona kama miaka imepita mingi hawajaenda unaona kama kuna ugonjwa unakuja hatari hatari wanakwenda pale na kuchukua mitambiko tambiko wanakuja kufanyia
Nyamgamba: haha au mvua mnaweza kuomba?
Mwita: eeh hata siku hiyo wakiomba inakuja tu
Nyamgamba: ooh inakuja tu
Mwita: eeh inakuja, wakati wa kiagazi tena inanyesha
Nyamgamba: sasa mlifanya hii mara ya mwisho ni mwaka gani?
Mwita: sikumbuki hapo, ilikuwa mimi ungali vado mdogo sana
Nyamgamba: ooh kweli na hawajafanya tena?
Mwita: hata ndio miaka yetu tunaterejea hawa twende
A: {kilugha}
Mwita: {kilugha}
Nyamgamba: mnasema?
A: mitambiko ya nyumbani ndio abahiri tuliyo fanya pale wanafuatwa tu
Nyamgamba: haha hii ya mojamaja
Mwita: eeh hii ya mojamaja
Nyamgamba: lakini hii ya wote?
A: inafanyika mara moja tu, kwa karne tuliyo nayo sasa hivi
Nyamgamba: ian jina maalum kama wote wanaenda
Mwita: jina maalum tunakwenda kusengera kwetu sasa
Nyamgamba: haha haina kwa kilugha haina jina kwamba wote wanaenda?
Mwita: ni wote wanakwenda hakuna kilugha
Nyamgamba: aah sawa
Mwita: kusengera
A: lugha ni kusengera
Nyamgamba: aah sawa lakini nilifikiri labda ni tofauti na ile nyumba ndogo ndogo kufanya kwenda
A: aah ile nyumba ndogo haiendi kusengera inafuata korosho

Mwita: au mwingine anaenda kufanya mitambiko ya nyumbani
Nyamgamba: ianfuataje hiyo korosho?
Mwita: inafuata pale majani, kufuata maji, kufuata nini
Nyamgamba: aah sawa haha sawa na ukisema hizi nyumba ambazo zinagawanyika huko si maana ya nyumba ni wake wa watu kila mke ana nyumba yake?
Mwita: hapo tumeshataja umeona hii majina hayo yote kama ni kisima kikubwa chetu cha Sengere ni wote halafu inawezekana kuwa kuna jiwe lingine linakuwa la wa kiseru wenyewe wanakwenda kwa niwe lao
Nyamgamba: hizi ambazo umetaja ni jiwe?
Mwita: eeh ni majiwe sasa inafuata milango milango
Nyamgamba: hiyo remande roma?
Mwita: remande ni jiwe
Nyamgamba: ni jiwe na roma?
Mwita: roma ni lijiwe, lina maji
Nyamgamba: aah ina maji
Mwita: madimbwi madimbwi, vidimbwi vya kuweza kuchotea maji
Nyamgamba: na tena rematomano?
Mwita: rematomano vilevile ni lijiwe limetambaa sasa lina kashimo
Nyamgamba: haha na tena ina maji
Mwita: eeh na maji yamo
Nyamgamba: na sengere?
Mwita: sengere ni mto sasa, kisima, nyaute ni jiwe lina maji
Nyamgamba: haha
Mwita: nyagikenge ni jiwe lina bwawa kule ndani
A: lina bwawa
Mwita: {Kilugha}
Nyamgamba: na yote ipo karibu karibu?
Mwita: eeh ipo karibu
Nyamgamba: kwahiyo ni kwenye milima hiyo?
Mwita: kwenye milima hizi
Nyamgamba: ooh nyuma yake?
Mwita: eeh nyuma yake huko juu, imesimama juu, niliona taa inawaka
Nyamgamba: ooh ulimwona
Mwita: niliona taa inawaka nikasema koroboi nini kumbe ilikuwa gari {kilugha} kama kuna taa unaona kule
A: {kilugha}
Mwita: unapotea kama hujui
Nyamgamba: aaah
Mwita: kama hujui unaweza ukapotea kabisa
Nyamgamba: ukienda huko?
Mwita: sasa mimi mwenyeji nitapoteaje na najua misimu iko hapo, watu wanapaogopa sana, sio mchezo
Nyamgamba: ooh hawaendi huko ovyo
Mwita: ooh kama hujui unaweza ukaangukia humo

Nyamgamba: ooh kwahiyo zamani watu walikuwa wamejenga huko?

Mwita: walikuwa wanakaa hukohuko mlimani

Nyamgamba: aah karibu na zile visima?

Mwita: vyote visima hivyo, watu walikuwa mlemle tu, akina baba wamezaliwa ni hukohuko akina mama sasa ndio wakaja kuhama wakati huu

Nyamgamba: haha walikuwa wanakaa juu ya milima

Mwita: juu ya milima, kama mnafanya ngome ni ngome hapo

Nyamgamba: vado zinaonekana

Mwita: eeh

Nyamgamba: aah

Mwita: {kilugha}

Nyamgamba: ni kama ngapi huko?

Mwita: {kilugha}

Nyamgamba: aina mbili

Mwita: eeh

Nyamgamba: ya nini?

Mwita: tatu {kilugha}

A: mlima moja una bugo mbili halafu mwingine ndio una mmoja

Nyamgamba: mmh#aah kumbe na ni enzi za akina nani walikuwa wamekaa huko?

Mwita: walikuwa ni enzi za akina babu zangu waliozaa baba

Nyamgamba: abasahi?

Mwita: abasahi

Nyamgamba: abanyambureti walikaa?

Mwita: ndio wanyambureti sasa ndio wamekaa sasa wanahamia kuja huku chini

Nyamgamba: aah na hawa abamaina ambao?

Mwita: wagamnyeri sasa ndio tuli..

Nyamgamba: hawa baba wa abasahi?

Mwita: walikuwa wanaishi sasa humuhumu

Nyamgamba: walikuwa wanaishi?

Mwita: mwenye mlima

Nyamgamba: aah kwahiyo ni akina nani walijenga ubugo?

Mwita: sitatambua

Nyamgamba: lakini unajua kwamba wamaina walikaa pale?

Mwita: wamaina walikaa humu, wasai walikaa humu sasa sijui ni akina nani waliona hiyo vita wakaanza kutengeneza lile ngome siwezi kufahamu,

A: lakini kwenye zile nani zangu kuna sehemu inayosema wanaanza kutengeneza kuzuia maana ubugo unaanza kujengwa kwenye mwaka elfu moja mia nane na, kipindi cha kuzuia wamaasai

Nyamgamba: mmh ndio haha

A: ukiangalia humo utapata hizo

Mwita: yeah ndiyo

A: kipindi hicho wanaanza kutumia ugwe

Nyamgamba: haha ugwe

Mwita: eeh ugwe

Nyamgamba: ni nini

A: ugwe ndio ubugo

Nyamgamba: aah ni moja?

A: eeh kiswahili ndio inaitwa ugwe

Nyamgamba: haha

Mwita: hiyo ngome

Nyamgamba: ugwe haha

A: eeh kiswahili sasa ndio walianza kuitumia na pamoja na wakaja kutumia tena haya, sijui inaitwaje

Mwita: {kilugha}

A: ni yale mamiti ambayo yanaota kwenye#{kilugha}

Nyamgamba: mmh cactus

A: inaitwa huwa inazaa watoto wakiiva ndani yake ni matunda mazuri sana

Nyamgamba: aah ni cactus

Mwita: ndiyo

Nyamgamba: walianza kufanya nini nayo?

Mwita: kufanya tena kama zizi kuzuia wasiingile na wamasaa na wanyama wakali

Nyamgamba: na ebogwo ni nini?

Mwita: ebogwo sijui

Nyamgamba: sijapata ile jina vizuri, hizi inaitwa nini?

Mwita: chingoto

Nyamgamba: abitoha

Mwita: aah hiyo hapana, kiswahili hii inaitwa marangali

A: unaona majani yake yapo hivi makubwa namna hii halfu yana miba miba

Nyamgamba: yeah

Mwita: yapo kwenye ukienda mediterrenean utaipata

A: inazaa watoto halafu yenyewe

Nyamgamba: yeah nimeipata kwahiyoy walikuwa wanaitumia kwa kufanya

Mwita: kuzuia kwenye vita

Nyamgamba: kwenye ubugo?

Mwita: haha wakati wa ubugo ni ubugo

Nyamgamba: haha

Mwita: halafu hiyo sasa ikatokea mamiba yakaja

Nyamgamba: haha

Mwita: {kilugha}

Nyamgamba: nasikia kwa wazee wengine kwamba sijui ni wakati wa abasahi au abanyambureti walikuwa na njaa kubwa sana wengine wanaita njaa ya mogoro

Mwita: eeh njaa ya mogoro eeh ilikuwepo ya abasahi hapa

Nyamgamba: ya abasahi?

Mwita: mmh njaa ya mogoro

Nyamgamba: walikuwa vado wanaishi pale?

Mwita: kwenye milima huku

Nyamgamba: haha lakini ilikuwa wajerumani bado au walikuwa wameshafika?

Mwita: aah wajerumani aah sasa hapo sitambui ilikuwa wajerumani au waarabu, maana wakati huu haukuwa na mtu wa kuandika mambo kama hayo, wanasema wasai walikuwa na hiyo njaa ya mogoro

Nyamgamba: haha wakaenda kuenea wapi?

Mwita: wengine wanakwenda Ukerewe

Nyamgamba: Ukerewe?

Mwita: eeh Ukerewe ndio walikwenda kufanyia, Ukerewe wanaleta viazi hapa..watu wanatoroshwa hapa na wakerewe kuenda usimbiti wanaingia Musoma

Nyamgamba: haha

Mwita: sasa mtu anasema nimevuka bahari sijui mto kumbe yuko hapahapa

Nyamgamba: na ugonjwa wa ile mogoro ilikuwa ndui?

Mwita: nini?

Nyamgamba: ambao walipata wakati wa ile njaa ya mogoro?

A: chebundi

Mwita: aah ndui

A: ndui au ndui si ndio gorondo

Mwita : eeh

A : malale si imetokea hapa, hii imetokea hapahapa wameham wamekuja hata mimi nina macho nimeona

Nyamgamba: yeah malale ni baadaye haha

A: ugonjwa uliotokea baada ya njaa ni ndui..

Mwita: gorondo ni

A: na kolera

Mwita: na kuhara watu walihara

A: nini si yellow fever ni kolera, hasahasa huu ugonjwa tunaouita sasa hivi ni kipindupindu

Nyamgamba: mmh

A: eeh maana watu walikuwa wanaharisha maji wanakufa

Mwita: hiyo iliua watu sana kwenye njaa

Nyamgamba: mmh ulisema kuna kipindi waarabu walikuwepo?

Mwita: si waarabu walifukuzwa na mjerumani

Nyamgamba: sawa waarabu walikuwa hapa wenyewe?

Mwita: eeh sasa walikuwa hapa waarabu ndio wakaja wakatawala wajerumani wakaja wakamfukuza

Nyamgamba: lakini utawala wao si ilikuwa si ni biashara tu au walikuja kufanya nini?

Mwita: sasa walikuja kibiashara na utawala humu

Nyamgamba: aah

Mwita: wanasema hakikisha unakuwa muislamu halafu wanaanza kuchapa watu karanga na sumu

Nyamgamba: mmh karanga, wanataka wapate karanga?

Mwita: eeh biashara

Nyamgamba: aah na walichukua watumwa?

Mwita: eeh ndio walikwenda na watu Magorondo, walikuwa wanachukulia mizigo yao wanakimbia wanapitia Ikoma huko wanakwenda huko

Nyamgamba: kwahiyo watu ambao walichukua ni hawa wa kubeba vitu vyao?

Mwita: mizigo eeh

Nyamgamba: aah

Mwita: walikuwa wanachukua mizigo

Nyamgamba: kwahiyo hawakuchukua kama watumwa watu wa kuwapeleka na kuwauza?

Mwita: hata hapa ilikuwa ni mizigo tu, hawakufika hapa

Nyamgamba: hawakufika?

A: aah wajerumani..waarabu

Mwita: waarabu?

A: huku hawakufika..{kilugha}

Mwita: {kilugha}

Nyamgamba: abasumba?

A: masumba si ni wajerumani

Nyamgamba: amasumba ni wajerumani, aah kumbe kwahiyo wengine wanachanganya wanaona hawa ni waarabu lakini sio?

Mwita: wote walikuwa ni rangi nyeupe..abasumba

Nyamgamba: amasumba hii neno ina maana gani?

Mwita: hii unajua hii wasumba imeteremka kipindi ambacho wasumba ni watu wanaopenda urafiki

Nyamgamba: aah

Mwita: na wale watu walikuwa wanakuja kiurafiki, wajerumani

Nyamgamba: walikuja kirafiki?

Mwita: eeh kwa mara ya kwanza walikuja kirafiki

A: walikuwa wanawadanganya hawa wakubwa wakubwa wengi kwamba mtufanyie hivi tupate hivi tupae hivi, kama wewe ulivyokuja sasa si umekuja kiurafiki?

Nyamgamba: mmh

Mwita: huwa wanaleta ushanga na vitu tofauti, nadhani wakawateka, huyu anasema nani ana meno ya tembo mwingine pembe ya faru wanawadanganya danganya hivi wakawaletea chuma, unajua watu wa zamani walikuwa wanataka vyuma vya shamba wanafurahi tu kumbe wanakwenda nao

Nyamgamba: hahana ninyi mlikuwa mnaua tembo kwahiyo mlikuwa na meno yao?

Mwita: tembo walikuwa wanauwawa hapa kwa wandorobo na wapo wangoremi waliokuwa wanapiga tembo vilevile wanafuga meno sasa wakawa wanawauzia

Nyamgamba: aah kumbe aah sawa kwahiyo wajerumani walipofika kutawala walifanyaje ili wapte huyu mtemi wa kwanza?

Mwita: hapo sasa sijui nilikuwa bado sijazaliwa

Nyamgamba: aah hukupata jinsi walivyo?

Mwita: aah sikupeleleza walifanyaje hapo

Nyamgamba: mmh sawa

Mwita: mwalimu anaweza akafahamu

A: eeh mjerumani hapa kwetu unajua hapa walipita

Nyamgamba: walipita tu?

A: mwaka 1916

Nyamgamba: haha

A: walikuwa wanakimbia

Mwita: {kilugha}

A: huwa walikuwa wanapita wanakimbia

Nyamgamba: haha lakini walipoweka watemi wao ndipo waliwatawala?

A: hata hawakufika huku kwetu, walikuwa bado

Mwita: ooh

Nyamgamba: ilikuwa kwahiyo watemi walikuwa..

Mwita: nchi ilikuwa iko chini ya mjerumani lakini na mtu yoyote aliyekuwa kwa kipindi hicho anatawala alikuwa chini ya uongozi wa kijerumani, kiinchi

Nyamgamba: sawa wenyewe

Mwita: lakini wajerumani wenyewe kufika walikuwa hamna, walikuwa bado ila wamepita sasa kipindi wanakimbia walipita hata ukienda kule Mguteni utakuja kukuta walipita halafu fedha yao noti zilifika mwaka 1916 na watu walitairi wanaita hizi vinoti

Nyamgamba: aah sawa eeh vizuri

Mwita: halafu hata hawa wenye sandeko ndio wajerumani walipita wenye sandeko hawa wakawa wanabeba yale masanduku

Nyamgamba: haha

Mwita: mizigo yao hiyo

A: {kilugha}

Mwita: kama kuna mtu amekwambia kwamba kuna keha {kilugha}

Nyamgamba: yeah

Mwita: kumbuka hapo usidanganywe baba kwasababu hii tohara ya kampuni ni kipindi kile wajerumani wameanzisha utawala wao kimakampuni

Nyamgamba: mmh

Mwita: kutoka mpaka Afrika ya kusini

Nyamgamba: sawa

Mwita: ndio tukafomu jina abakabwe unaona, tukahama pale tukaja mwenye sandeko hicho kipindi ambacho wajerumani wakawa wanaondoka

A: kampuni hiyo kama ulisikia akina mama yangu walikuwa na vinoti

Mwita: vinoti ni kipindi wametoa nini, wametoa hizo noti zao za kwanza mwaka 1915#

Nyamgamba: haha sawa kwahiyo naomba mzee..

{THE END OF TAPE # 160, DONE BY NYAMUSI MAGATTI, AUGUST, 2009}